# JARIDA LA USHIRIKA

Together We Build Our Economy

ISSN 2714 - 2175 Toleo Na. 19

Oktoba - Desemba 2025



## BIMA YA USHIRIKA KUANZISHWA

# KUTOKA KWA MRAJIS



***Dkt. Benson Ndiege, Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC***

Niwakaribishe tena katika Jarida hili Toleo la 19 ambalo linatupa fursa ya kupata Habari, matukio na elimu ya masuala mbalimbali katika sekta ya Ushirika katika kipindi cha Oktoba – Desemba 2025.

Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) vimeonesha mafanikio makubwa katika siku za hivi karibuni yameoneshwa Dhahiri katika taarifa ya Utendaji wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo 2024 Toleo la nne lililozinduliwa mwishoni wa mwezi Septemba 2026.

Taarifa hiyo imebainisha mafanikio mbalimbali yaliyopatikana, Hivyo ili kuimarisha na kuendeleza Ushirika huo wa Kifedha Serikali imekuwa ikitoa maelekezo yanayolenga kulinda ustawi wa Vyama hivi ikiwa ni Pamoja na kuzielekeza SACCOS zote kufunga Hesabu ifikapo mwisho wa Mwaka. Kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika na Huduma Ndogo za Fedha Mwaka wa Fedha wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) huanza Mwezi Januari na kuisha Mwezi Desemba kila mwaka.

Kwa kuzingatia matakwa hayo, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), huzitaka SACCOS zote kuhakikisha zimefunga Hesabu zake za Mwaka husika kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 55(2) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013, Kifungu cha 47 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha za Mwaka 2018 na kanuni ya 55 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015 na kutakiwa kuziwasilisha kwa Mkaguzi wa Nje Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) au Mkaguzi mwingine aliyeidhinishwa.

Katika kutekeleza matakwa haya ya Sheria na Kanuni, Mrajis anawaelekeza Viongozi wa SACCOS nchini kuhakikisha wanafunga Hesabu za Mwaka 2025 ili hesabu hizo ziweze kukaguliwa na kurudishwa kwao mapema.

Baada ya hatua hiyo Viongozi wa SACCOS wanapaswa kujibu hoja zote zilizotolewa na zitakazotolewa na Wakaguzi ili kuondokana na uwepo wa Hati mbaya pamoja na Hati chafu. Chama kitakachoshindwa kujibu hoja husika na kupata hizo au hasara, Viongozi na Watendaji wake watapaswa kuwajibika kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 55(13) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika, kanuni ya 85(g) ya Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) za Mwaka 2019.

Tume inaendelea kusisitiza SACCOS kuzingatia Ufungaji wa Hesabu kwa wakati ili kuendana na matakwa ya Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika.

ISSN 2714 - 2175 Toleo Na. 19



# YALIYOMO

1. KUTOKA KWA MRAJIS.........................................................................................................................i

2. BIMA YA USHIRIKA KUANZISHWA; COASCO KUENDELEA NA UKAGUZI WA VYAMA..........................1

3. SACCOS NGUVU YA UCHUMI - NAIBU KATIBU MKUU HAZINA..........................................................3

4. TCDC SACCOS YAPOKEA CHETI NA ZAWADI KUTOKA BENKI YA USHIRIKA ....................................4

5. VIJANA WAHAMASISHWA KUSHIRIKI SHUGHULI ZA USHIRIKA SONGWE .........................................5

6. BURUTE SACCOS LTD YATIMIZA MSINGI WA SABA WA USHIRIKA ....................................................6

7. TCDC NA TCJE ZAFANYA MAJADILIANO KUBORESHA USHIRIKA WA TUMBAKU...............................8

8. TSN YAIPONGEZA TCDC KWA USHIRIKIANO NA WADAU...................................................................9

9. WANACHAMA TCDC SACCOS WAUPONGEZA UONGOZI..................................................................10

10. USINDI AMCOS WANUNUA TREKTA KUENDELEZA KILIMO...............................................................11

11. USINDI AMCOS WATIMIZA MSINGI WA SABA WA KUJALI JAMII.......................................................12

12.TANECU YANUNUA MALORI YA KUSAFIRISHA MAZAO YA WAKULIMA...........................................13

ISSN 2714 - 2175 Toleo Na. 19



# BIMA YA USHIRIKA KUANZISHWA

## - COASCO KUTOA TAARIFA YA KINA KUHUSU UKAGUZI WA VYAMA KILA MWAKA



*Waziri wa Kilimo, Mhe. Daniel Chongolo, akipokea Taarifa ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika visivyo vya kifedha ya Mwaka 2025 toleo Na. 1 kutoka kwa Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) zimetakiwa kufanya kazi kwa kushirikiana na kuhakikisha ushirika unaimarika ikiwa ni pamoja na kuanzisha Bima ya Ushirika (COOP insurance) na ukaguzi wa maendeleo ya vyama vya ushirika.

Wito huo umetolewa na Waziri wa Kilimo, Mhe. Daniel Chongolo, wakati wa kikao kazi na Taasisi hizo tarehe 24 Novemba 2025.

Waziri Chongolo amepongeza pia hatua ya TCDC kutaka kutengeneza Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Ushirika akitaka uwe wa miaka 25 kuendana na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

"Tuweke utaratibu wa kuwa na matokeo kwa hatua, kwa mfano hadi kufikia mwaka 2030 tutekeleze tuliyojipangia kwenye Agenda 10/30 na hatimae mwaka 2050 kuwa na matokeo kwenye mpango huo kabambe tunaotaka kuutengeneza," amesema Waziri Chongolo.

Aidha, COASCO, imeelekezwa kutoa taarifa ya kina kila mwaka kuhusu ukaguzi wa vyama ambapo ataitolea

maelekezo kuelekea kwenye mikutano ya Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) kwa ajili ya utekelezaji. “Ukaguzi uwe asilimia 100 na kama tatizo ni rasilimali fedha tutatafuta vyanzo ili hii kazi itekelezeke kuleta tija zaidi,” amesema Waziri Chongolo.



Kikao kazi hicho kiliwahusisha pia na Mhe. David Silinde, Naibu Waziri wa Kilimo; Gerald Mweli, Katibu Mkuu na Mh. Athumani Kilundumya, Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Ushirika na Umwagiliaji, Mrajis wa Vyama vya Ushirika; Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa COASCO na Menejimenti ya Wizara ya Kilimo.



*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege, akitoa Taarifa ya TCDC*



*Kaimu Mtendaji Mkuu wa COASCO, CPA. Jeremiah Mugeta akitoa Taarifa ya COASCO*

ISSN 2714 - 2175 Toleo Na. 19 Oktoba - Desemba 2025

# SACCOS NGUVU YA UCHUMI - NAIBU KATIBU MKUU HAZINA



*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege, akimkabidhi Naibu Katibu Mkuu - Hazina, Elijah Mwandumbya, Taarifa ya maendeleo ya Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) ya Mwaka 2024 toleo Na. 4, katika uzinduzi wa taarifa hiyo Jijini Arusha*

Naibu Katibu Mkuu - Hazina Elijah Mwandumbya amesema Serikali itaendelea kuimarisha na kusimamia Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) ili viweze kuchochea kasi katika shughuli za kiuchumi za Wananchi.

Amesema hayo wakati wa Uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS), kwa mwaka 2024 yaliyofanyika Septemba 29, 2025 Jijini Arusha.

Akiwasilisha Taarifa hiyo Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege amesema Taarifa hiyo inaonesha kukua kwa Ushirika wa Akiba na Mikopo nchini.

Ukuaji huo ulibainishwa na vigezo mbalimbali vilivyotumika ikiwemo Mali za SACCOS kuongezeka kutoka Shillingi Trillioni 1.32 mwaka 2023 hadi Trillioni 1.46 mwaka 2024.

Amesema Utoaji wa Mikopo umeongezeka kutoka Shillingi Trillioni 1.1 mwaka 2023 hadi kufikia Trillioni 1.20 mwaka 2024.

Uzinduzi huo umehudhuriwa na wawakilishi wa Taasisi mbalimbali ikiwemo Wizara ya Kilimo, Benki Kuu ya Tanzania, SCCULT, MoCU, TFC, COASCO, DSIK pamoja na SACCOS husika.

# TCDC SACCOS YAPOKEA CHETI NA ZAWADI KUTOKA BENKI YA USHIRIKA



*Viongozi wa TCDC SACCOS (kushoto) na Kitengo cha masoko (kulia) kutoka Benki ya Ushirika katikia makabidhiano ya zawadi na cheti kutoka Benki katika ofisi za TCDC SACCOS, Jijini Dodoma*

Chama cha Akiba na Mikopo cha TCDC SACCOS kimepokea cheti na zawadi kutoka Benki ya Ushirika kutokana na uwekezaji waliofanya katika Benki hiyo



# VIJANA WAHAMASISHWA KUSHIRIKI SHUGHULI ZA USHIRIKA SONGWE




*Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mhe. Jabiri Makame, akizungumza na Vijana walioshiriki Bonanza lililoandaliwa na SORECU LTD, Mkoani Songwe*

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mhe. Jabiri Makame, ameongoza bonanza linalohamasisha Vijana kushiriki shughuli za Ushirika lililofanyika Mkoani humo Oktoba 16, 2025.

Mhe. Makame amesema hayo katika bonanza lililoandaliwa na Chama Kikuu cha Ushirika Mkoani Songwe (SORECU LTD).

Naye Ofisa Operesheni wa SORECU, Moni Mwampamba, alisema bonanza hilo lilikuwa na lengo la kuhamasisha Vijana kutumia Nishati Safi, kulinda mazingira na kushiriki katika shughuli za kilimo na Ushirika. Moni aliyazungumza hayo katika kilele

Bonanza hilo ni sehemu ya Jitihada za SORECU kuunganisha Vijana kupitia michezo na elimu ya uhifadhi wa Mazingira ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara bila kuathiri ekolojia ya mkoa huo.



*Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mhe. Jabiri Makame, akizungumza na Vijana walioshiriki Bonanza lililoandaliwa na SORECU LTD*

# BURUTE SACCOS LTD YATIMIZA MSINGI WA SABA WA USHIRIKA



*Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mhe. Fatma Mwassa, akiwakabidhi wanafunzi baadhi ya vitu vilivyotolewa kama msaada vilivyotolewa na Chama cha Ushirika BURUTE SACCOS*

BURUTE SACCOS LTD imetimiza msingi wa Saba wa ushirika ambao ni kujali jamii katika Wilaya za Bukoba na Missenyi mkoani Kagera.

Tukio hili limehudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa Kagera, Mhe. Fatma Mwassa, ambaye amekuwa Mgeni rasmi katika tukio hili, ambapo ameweza kupokea misaada ya vitu mbalimbali kama Madawati 340, bima za afya Kwa wanafunzi 40,vyandarua 205 , sukari kilo 100, pampas za watoto wadogo



boksi 6, maharage kilo 200, blanketi na mashuka 240, pia shilingi 1,000,000 kwa kituo cha kulelea watoto na ameweza kukabidhi vitu hivyo kwa wakuu wa Wilaya za Missenyi na Bukoba kwa ajili ya kugawa katika Wilaya hizo. Pia, Mhe. Mwassa ameipongeza BURUTE SACCOS LTD kwa kuendelea kutoa misaada mbalimbali ndani ya Wilaya za Bukobana Misenyi Mkoani Kagera na kutoa wito kupitia

Mrajis Msaidizi wa vyama vya Ushirika Mkoa Kagera, Enikia Bisanda kwa vyama vingine vya Ushirikakuigajambohililakujalijamii.

Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Erasto Sima, ameipongeza BURUTE SACCOS LTD kwa kuendelea kutoa misaada hiyo Kila mwaka Kwenye Wilaya hizo mbili.



Aidha, wanufaika wameweza kutoa shukuran zake Kwa BURUTE SACCOS LTD Kwa kuendelea kuigusa jamii ya Wilaya za Bukoba na Missenyi mkoani Kagera.




*Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Kagera, Enikia Bisanda, akizungumza na Wanaushirika wa BURUTE SACCOS LTD,*

# TCDC NA TCJE ZAJADILI KUBORESHA USHIRIKA WA TUMBAKU



*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege, akiongoza majadiliano kuhusu masuala mbalimbali ya ushirika wa Tumbaku kati ya TCDC na TCJE, kilichofanyika Jijini Dodoma.*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Mradi wa Pamoja wa Vyama vya Ushirika wa Tumbaku (TCJE) zimekutana katika kikao cha kujadili masuala ya utekelezaji wa maboresho ya Ushirika wa Tumbaku.

Kikao hicho kimefanyika Novemba 20, 2025 Jijini Dodoma ambapo masuala yaliojadiliwa ni pamoja na masuala ya Bima za mikopo, mjengeko wa bei ya Tumbaku, usambazaji na upatikanaji wa Pembejeo pamoja na usimamizi wa Rasilimali za Vyama vya Ushirika wa Tumbaku. kikao kiliongozwa Dkt. Benson Ndiege Mrajis na Mtendaji mkuu wa TCDC na TCJE iliwakilishwa na Meneja Mkuu Benedict Kisaka.



# TSN YAIPONGEZA TCDC KWA USHIRIKIANO NA WADAU



*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege, akipokea chapisho la Toleo maalumu la Pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), alipotembelewa na Mkurugenzi wa Maendeleo na Masoko wa TSN, Soter Salema, Jijini Dodoma.*

Kampuni ya magazeti ya Serikali (Tanzania Standard Newspapers - TSN) wachapishaji wa magazeti ya Daily News na Habari wameipongeza Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kwa kutambua mchango wake katika kushirikiana na wadau ikiwemo Sekta ya Habari nchini na kuwa mdhamini katika matukio mbalimbali ya kitaifa.

Pongezi hizo zimetolewa Novemba 14, 2025 Jijini Dodoma na Mkurugenzi wa Maendeleo na Masoko wa TSN, Soter Salema, wakati akikabidhi Toleo la Maalumu la Pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza katika tukio hilo, Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege, ameishukuru na kuipongeza TSN kwa kuendelea kutangaza Mafanikio ya Serikali katika miaka yote tangu Uhuru.



# WANACHAMA TCDC SACCOS WAUPONGEZA UONGOZI



*Mwenyekiti wa Mkutano, Aron Mrema, akiongoza mkutano mkuu wa TCDC SACCOS LTD, uliofanyika Jijini Dodoma*

Wanachama wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC SACCOS LTD) wametoa pongezi kwa uongozi wa TCDC SACCOS kwa kuendesha Chama hicho kwa uweledi mkubwa na kwa kuzingatia kanuni na sheria za Vyama vya Ushirika na hata kufika mafanikio makubwa hata kufikia mkutano Mkuu ikiwemo kupata hati inayoridhisha.

Wanachama hao wametoa pongezi hizo Novemba, 2025 wakati wa Mkutano Mkuu wa Tisa (9) wa mwaka uliofanyika Jijini Dodoma. Pongezi zilizotolewa kwa Chama ni pamoja na Chama kutengeneza faida ya shilingi milioni 46.4 kwa mwaka 2025 na mapato kufikia milioni 54.4 na kuwa na matumizi madogo yasiyozidi kiasi cha Shilingi milioni 10 kwa mwaka.

Aidha, Chama kimeongeza hisa zake kutoka Shilingi milioni 52.9 kwa mwaka 2024 hadi kufikia Shilingi milioni 64.4 kwa mwaka 2025 ikiwa ni ongezeko la asilimia 16 kwa mwaka.

Kwa upande wa Akiba zimeongezeka kutoka Shilingi milioni 316.2 kwa mwaka 2024 hadi kufikia shilingi milioni 494.4 kwa mwaka 2025 ikiwa ni ongezeko la asilimia 56

Akitoa taarifa ya Bodi ya Chama hicho Mwenyekiti wa TCDC SACCOS Ramadhan Miraji amesema Chama kitaendelea kuwahamasisha watumishi wa TCDC kujiunga na Chama hicho, kuhamasisha Wanachama kuendelea kuweka Akiba na kukamilisha Mfumo wa TEHAMA utakaosaidia katika kuboresha ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Chama hicho.

Katika mkutano huo wajumbe wamekubaliana kuendelea kuweka Akiba, kuongeza huduma za upatikanaji wa Mikopo, kuongeza wanachama ili kuweza

# USINDI AMCOS WANUNUA TREKTA KUENDELEZA KILIMO



*Viongozi wa USINDI AMCOS LTD na Mrajis Msaidizi Mkoa wa Tabora,Venance Msafiri (kulia), wakifurahia jambo baada kufanya uzinduzi wa trekta iliyopnunuliwa na Chama hicho, Mkoani Tabora*

Chama cha Ushirika cha Msingi Usindi AMCOS Ltd cha Kaliua Mkoani Tabora kimenunua trekta kwa ajili ya shughuli za kilimo na pia watakodisha kujiongezea kipato.

Uzinduzi wa Trekta hilo umefanywa mwezi Desemba , 2025 na Katibu Tawala Wilaya ya Kaliua Sosthenes Chakupanyuka, katika Mkutano Mkuu wa kufunga mwaka wa Chama hicho. Sosthenes amewapongeza kwa hatua hiyo kubwa na kusema Usindi AMCOS ni chama cha mfano wa kuigwa kwa Kaliua kwa kutimiza vyema lengo lao la kununua Trekta yao ya pili. Ameahidi kuwa nao pamoja penye changamoto ashirikishwe.

Pia amefurahishwa sana na namna ambayo wamekuwa wakijali jamii kwani wameweza kutoa mifuko 100 ya Simenti kwa ajili ya kujenga shule,




kuweka umeme kwenye shule za Msingi na kujenga barabara ya kuelekea Zahanati ya Usindi.

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Tabora Venance Msafiri ameahidi kuwapeleka wakulima mafunzo kuongeza Elimu ya Kilimo na Madereva wa Matrekta kuongeza ujuzi. Msafiri amewapongeza Usindi AMCOS kwa kupata Hati Safi kwani ni miongoni mwa Vyama vichache vilivyoweza kufika hatua hiyo.

# USINDI AMCOS WATIMIZA MSINGI WA SABA WA WA KUJALI JAMII

Chama cha Msingi Usindi AMCOS Ltd cha Kaliua Mkoani Tabora katika kutelekeza msingi wa saba wa Ushirika wamerudisha shukrani kwa jamii

Hayo yamefanyika katika vituo viwili ambavyo ni Istiqaama kilichopo kata ya Malolo Halmashauri ya Tabora na Mama Tereza wa Kalikuta Tabora.

Mmoja wa Walezi hao, Sista Maria Rosaria amewashukuru Usindi AMCOS na timu nzima ya Ushirika kwa upendo mkubwa wa kujitoa kila mwaka.

Mrajis msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoani Tabora Venance Msafiri na Mrajis msaidizi sehemu ya Uhamasishaji na Uratibu Dodoma Ibrahim




*Viongozi wa USINDI AMCOS LTD, wakikabidhi vitu mbalimbali katika vituo vya Istiquama na Mama Tereza wa Kalikuta, Kaliua Mkoa wa Tabora*

Kadudu, wameipongeza Usindi AMCOS kwa kutekeleza msingi wa saba wa Ushirika kila mwaka na kutoa wito kwa Wanaushirika kuiga mfano huo mzuri.



Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Tabora, Venanci Msafiri na Viongozi wa Usindi AMCOS, wakizungumza na watoto katika kituo cha kulelea watoto yatima ISTIQAMA

# TANECU YANUNUA MALORI YA KUSAFIRISHA MAZAO YA WAKULIMA



Malori ya Chama Kikuu cha Ushirika TANECU LTD yaliyo nunuliwa kwa ajili ya usafirishaji mazao ya wakulima

Chama Kikuu cha Ushirika cha TANECU LTD kimezindua malori mapya matano yenye thamani ya shilingi bilioni 1.005 hatua inayolenga kuongeza ufanisi katika usafirishaji wa korosho za wakulima kwa msimu huu na misimu ijayo.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi iliyofanyika wilayani Tandahimba Meneja Mkuu wa TANECU LTD Mohamed Mwinguku Amesema malori hayo yenye uwezo wa kubeba tani 32 kila moja yamenunuliwa kwa mkopo kutoka Benki ya NBC, ikiwa ni sehemu ya mpango mpana wa chama hicho wa kumiliki jumla ya malori 50.

"Tumekamilisha awamu ya kwanza kwa kununua malori haya matano. Huu ni mwanzo wa safari yetu ya kuwa na malori 50 yatakayorahisisha usafirishaji wa korosho na kupunguza gharama tulizokuwa tunapata kutokana na kukodisha magari," alisema Mwinguku.

# TCDC KUSHIRIKIANA NA WADAU MBALIMBALI KUENDELEZA USHIRIKA




*Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)*
*Mtaa wa Kuu, S. L. P. 201, DODOMA.*
*Simu: +255 26 23 22456, Telefax: +255 26 23 21973*
*Barua Pepe: ushirika@ushirika.go.tz Tovuti: www.ushirika.go.tz*
*ushirika_tcdc*   *Tume ya Maendeleo ya Ushirika*